REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THE HANSARD

Tuesday, 16th October, 2018

The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2.30 p.m.

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

MOTION

ADOPTION OF THE REPORT ON KILIFI COUNTY FOREST POLICY, 2018

Hon. Hassan: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Leo ikiwa ni Jumanne tarehe 16 Oktoba mwaka 2018 naomba kuhamasisha Hoja ya kwamba Bunge hili likubali Ripoti ya Kamati ya Maji, Mazingira na Mali Asili ya sera ya msitu ya Jimbo la Kilifi, 2018 iliyowekwa kwenye jedwali la Bunge hili la heshima leo Jumanne tarehe 16 Oktoba.

Asante sana mheshimiwa Spika. Ningeliomba kuchukua nafasi hii kumuomba mheshimiwa Shaban aiunge mkono Hoja hii.

(Hon. Shaban seconded)

MOTION OF ADJOURNMENT UNDER STANDING ORDER 92

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Thuva?

Hon. Thuva: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. I stand on a Point of Order under Standing Order No. 92 about the Adjournment of a Motion on the Floor of the House. Mr. Speaker, we understand that we have not gotten enough time to go through this Report and that is why I am seeking for an adjournment of this Motion.

Again, Mr. Speaker, tomorrow we are having the Governor's address and it will be prudent, Mr. Speaker, to actually give Members ample time to prepare so that they can be able to be attentive on that day.

(Question proposed)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. Stanley Kenga.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Kenga: Asante mheshimiwa Spika, kwa nafasi uliyonipa ili pia kuweza kuchangia katika Hoja ambayo iko mbele yetu. Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuunga mkono Hoja ambayo imewezwa kuletwa na mheshimiwa Pascal Jacob Thuva kwa sababu zifuatazo.

Nimeweza kuangalia sera ambayo imeletwa kwetu na Mwenyekiti wa Kamati ambayo inahusiana na Maji, Mazingira na Mali asili na kwamba sera hii ya 2018 imeweza kujumuisha maswala mengi sana ambayo yanahusiana na mambo ya misitu, mambo ya mali asili na mambo ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, unapoangalia ukurasa wa 15 wa Ripoti ambayo iko mbele yetu kwa ajili ya kujadiliwa, utaona imegusia hata mambo ya Ukimwi na kuna maswala ambayo yanajitokeza ambayo ni maswala nyeti. Hivyo basi, kama leo ndio tumeweza kupata Ripoti hii ndani ya Bunge hili, sioni kwamba tuko na wakati mwafaka wa kuweza kuikagua kikamilifu ili tuweze kufanya uamuzi na mchango ambao utakuwa wa hekima kuhakikisha sera hii inapopita itakuwa imeweza kweli kushughulikia kikamilifu maswala yote ambayo tungehitaji yaweze kushughulikiwa.

Swala lengine mheshimiwa Spika, ni katika ukurasa wa 13 ambapo inaangazia mambo ya *Inter-County Cooperation*. Mheshimiwa Spika, utagundua kwamba katika eneo letu tumeweza kupakana na Kaunti nyingine na mbali na hizi gatuzi, kuna wale ambao wako na misitu katika maeneo yao; wengine hawana na ni lazima tuwe makini kuhakikisha ni vipi tutashirikiana. Unaposhirikiana na mtu ambaye hana raslimali na wewe uko nayo, mara nyingi huenda ukapata hasara. Kwa hivyo, ni lazima tuhakikishe kwamba sera hii tumeweza kuikagua kwa wakati.

Pia, tumeelezwa kwamba, kesho ni rasmi kuwa tutakuwa na *address* ya Gavana katika Bunge letu la Kilifi na tunahitaji wakati mzuri wa kuweza kujiandaa ili tuweze kupokea ile *address* ambayo mheshimiwa Gavana ataweza kuhutubia kwa sababu hili ni swala ambalo linahusiana na ni vipi serikali itaweza kujipanga ndani ya kipindi hiki; utendakazi na huduma kwa jamii. Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono tupate nafasi ya kuweza kuahirisha mkao huu ili tukapate wakati mzuri wa kuweza kujipanga. Asanteni.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you. Hon. Peter Ziro.

Hon. Ziro: Asante Mheshimiwa Spika. Nami nimesimama ili kuunga mkono Hoja hii muhimu ambayo mheshimiwa Pascal ameweza kuileta katika Bunge hili. Nilipokuwa napitia nakala hii, nimeona kuwa imetaja mambo ya misitu na ile Wadi yangu imepakana na msitu ule wa Tsavo na mara kwa mara nimeona athari za hiyo misitu hata ijapo ni mizuri kwa wananchi, lakini wakati mwengine kuna athari zake kwa sababu mara nyingi wanyama wa pori huvamia wananchi.

Hivi tunavyozungumza, kuna simba na kiboko ambao wamevamia Wadi ya Garashi na hivyo basi nahitaji wakati mzuri wa kuipitia hii Ripoti ili nielewe hii misitu ambayo imepakana na wananchi kama kuna mipangilio gani ambayo inaweza kufanywa ili kusudi athari hizi ambazo zinaletwa na hii misitu ziwe haziwezi kutokea.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono Hoja hii na vile kama wenzangu walivyotangulia kuzungumza kwamba kesho tuko na mheshimiwa Gavana ambaye atakuwa hapa na ni muhimu pia tuwe na maandalizi mwafaka ili anapokuja, akute nyumba yetu tumeitengeneza vizuri; waswahili walisema ‘mgeni njoo mwenye mji apone.’ Kwa hivyo, tujiandae ili kusudi Mheshimiwa Gavana akija, tuone tutapona vipi. Kuna maneno ambayo ni tuyazungumze na tukubaliane huyu ni mzee wa boma na anapokuja hapa tujue tutamkaribisha vipi na atakapoondoka na sisi tutapona vipi.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kwa hivyo, hayo ni mambo ambayo labda kama Bunge tuweze kuyaketia hapa tujue kwamba huyu ni mzee akija na sisi tutapona namna gani. Unajua kwamba hii hali ni ngumu sana na kila mmoja anajua. Mheshimiwa Sonko (Karisa) hata jana hakuwa hapa; mambo yalikuwa mabaya sana kule kwake. Ameingia leo na nafikiri yeye anaweza kuongoza hili Bunge katika kuangalia vile mheshimiwa Gavana atakavyofanya Bunge hili lipone. Kwa hayo machache mheshimiwa Spika, nasema asante sana.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Ziro, I will make sure I send your message today *"kwamba mgeni njoo mwenyeji apone"*.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Hon. Members, in the absence of any other Business in the Order Paper, I move to adjourn this House until tomorrow in the afternoon. Thank you.

The House rose at 2:41 p.m

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*